



# TANZANIA BUREAU OF STANDARDS (TBS)



## HAND BOOK 2026



## YALIYOMO

**UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU..... III**

**MAANA ZA VIFUPISHO ..... IV**

**1.0 UTANGULIZI ..... 01**

1.1 Utambulisho..... 01

1.2 Dira ..... 01

1.3 Dhima..... 01

1.4 Majukumu..... 01

1.5 Viwango..... 02

1.5.1 Kiwango ni nini? ..... 02

1.5.2 Viwango hutayarishwaje? ..... 02

1.5.3 Faida za viwango ..... 03

1.5.4 Wapi na jinsi gani naweza kupata kiwango cha  
Tanzania? ..... 03

**2.0 HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA SHIRIKA LA**

**VIWANGO..... 04**

2.1 Huduma ya Udhhibiti Ubora..... 04

2.1.1 Matumizi ya alama ya ubora ya TBS ..... 04

2.1.2 Cheti cha Ubora ..... 04

2.1.3 Huduma ya uthibitishwaji mifumo ya usimamizi  
wa Ubora..... 05

2.2 Upimaji na Metrolojia..... 06

2.2.1 Maabara ya Kemia ..... 06

2.2.2 Maabara ya Uhandisi Ujenzi ..... 07

2.2.3 Maabara ya Uhandisi Mitambo ..... 07

2.2.4 Maabara ya Uhandisi Umeme ..... 07

2.2.5 Maabara ya Kemia ya Chakula ..... 07

2.2.6 Maabara ya Mikrobiolojia ..... 07

2.2.7 Maabara ya Pamba, Ngozi na Nguo ..... 08

2.2.8 Kituo cha Teknolojia ya Ufungashaji..... 08



|            |                                                                                  |           |
|------------|----------------------------------------------------------------------------------|-----------|
| 2.2.9      | Maabara ya Metrolojia Jotoridi, Umeme ,<br>Muda na Masafa .....                  | 09        |
| 2.2.10     | Maabara ya Metrolojia ya Tungamo na<br>Vipimo vinavyohusiana .....               | 09        |
| 2.2.11     | Maabara ya Metrolojia ya Urefu.....                                              | 09        |
| 2.2.12.    | Maabara ya Metrolojia ya Kemikali .....                                          | 10        |
| 2.3        | Mafunzo na Ushauri .....                                                         | 10        |
| 2.4        | Usajili wa majengo ya chakula na vipodozi.....                                   | 10        |
| 2.5        | Usajili wa bidhaa wa chakula na vipodozi.....                                    | 10        |
| <b>3.0</b> | <b>UTARATIBU WA KUPATA ALAMA YA UBORA .....</b>                                  | <b>11</b> |
| 3.1        | Hatua ya Kwanza – Maombi .....                                                   | 11        |
| 3.2        | Hatua ya Pili – Ukaguzi wa Awali .....                                           | 11        |
| 3.3        | Hatua ya Tatu – Upimaji .....                                                    | 11        |
| 3.4        | Hatua ya Nne – Utoaji wa Leseni .....                                            | 11        |
| 3.5        | Muda wa leseni ya alama ya ubora .....                                           | 12        |
| 3.6        | Gharama kwa wajasiriamali wadogo na wa kati .....                                | 12        |
| <b>4.0</b> | <b>UTARATIBU WA USAJILI WA BIDHAA NA MAJENGO YA<br/>CHAKULA NA VIPODOZI.....</b> | <b>13</b> |
| <b>4.1</b> | <b>UTARATIBU WA USAJILI WA BIDHAA.....</b>                                       | <b>13</b> |
| 4.1.1      | Hatua ya Kwanza – Maombi .....                                                   | 13        |
| 4.1.2      | Hatua ya Pili – Malipo .....                                                     | 13        |
| 4.1.3      | Hatua ya Tatu – Tathimini.....                                                   | 13        |
| 4.1.4      | Hatua ya Nne – Usajili .....                                                     | 13        |
| <b>4.2</b> | <b>UTARATIBU WA USAJILI WA MAJENGO.....</b>                                      | <b>14</b> |
| 4.2.1      | Hatua ya Kwanza – Maombi .....                                                   | 14        |
| 4.2.2      | Hatua ya Pili – Malipo .....                                                     | 14        |
| 4.2.3      | Hatua ya Tatu – Tathimini.....                                                   | 14        |
| 4.2.4      | Hatua ya Nne – Usajili .....                                                     | 14        |
| <b>5.0</b> | <b>ORODHA YA BIDHAA ZILIZOIGWA MARUFUKU.....</b>                                 | <b>15</b> |
| <b>6.0</b> | <b>UKAGUZI WA BIDHA NJE YA NCHI.....</b>                                         | <b>16</b> |
| <b>7.0</b> | <b>HITIMISHO .....</b>                                                           | <b>17</b> |

## UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU



Kwa niaba ya wafanyakazi wa Shirika la Viwango Tanzania, kwa heshima na taadhima, napenda kuwakaribisha wote katika Shirika la Viwango Tanzania, “Nyumbani kwa viwango”. Kitabu hiki kinafafanua kwa mapana, kazi, majukumu na huduma za Shirika, ambapo viwango na udhibiti ubora ni kipaumbele cha Shirika. Pia kitabu hiki kinatoa elimu ya jumla kuhusu Shirika la Viwango Tanzania, nini Shirika linafanya na wapi linaelekea.

Asante kwa kuwa sehemu ya familia yetu na tunatumaini kwamba utafurahia kusoma kitabu hiki na kitakuwa msaada mkubwa kwako.

**Dkt. Ashura A. Katunzi**  
Mkurugenzi Mkuu  
Shirika la Viwango Tanzania (TBS)





## MAANA ZA VIFUPISHO

|       |                                            |
|-------|--------------------------------------------|
| HACCP | Mfumo wa Usimamizi wa Usalama wa Chakula   |
| ICS   | Uainishaji wa Viwango Kimataifa            |
| ISO   | Shirika la Viwango la Kimataifa            |
| PTC   | Kituo cha Teknolojia ya Ufungashaji        |
| SIDO  | Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo |
| TBS   | Shirika la Viwango Tanzania                |

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Utambulisho

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ni Shirika la umma chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara liloundwa chini ya Sheria ya Bunge Na.3 ya Mwaka 1975, n kuanza kazi rasmi Mwaka 1976 ambapo lilipewa jukumu la kuratibu uandaaji wa viwango na kusimamia utekelezaji wake kupitia Sheria ya Viwango Sura Na.130

### 1.2 Dira

Kuwa ofisi inayoongoza barani Afrika katika viwango, ubora na usalama

### 1.3 Dhima

Kukuza viwango na kutoa huduma za uhakikisho wa ubora zinazowalinda watumiaji, kurahisisha biashara na kuongeza ushindani wa soko wa bidhaa na huduma za Tanzania.

### 1.4 Majukumu

Shirika lina majukumu mengi kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Viwango Sura namba 130.

1. Kutayarisha na kusimamia viwango vyote vya kitaifa
2. Kutoa ushauri viwandani juu ya uzalishaji wa bidhaa bora
3. Kupima na kuhakiki vipimo vinavyotumika viwandani
4. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa viwandani
5. Udhibiti wa bidhaa zenye ubora hafifu
6. Utoaji wa alama na cheti cha ubora wa bidhaa za ndani na nje ya nchi
7. Kuelimisha umma juu ya masuala yote yanayohusu



uwekaji na usimamiaji wa viwango pamoja na udhibiti ubora wa bidhaa viwandani

8. Ukaguzi na usajili wa majengo au maeneo kama machinjio, mabucha, maduka makubwa (supermarkets), maduka ya vyakula na vipodozi, wanaopika vyakula kwenye masherehe (caterers) mahoteli, maghala na maeneo ya uzalishaji
9. Usajili wa chakula na vipodozi

## 1.5 Viwango

### 1.5.1 Kiwango ni nini?

Kiwango ni mwongozo na maelekezo ya kitaalamu kwa wabunifu, watengenezaji na watumiaji wa bidhaa, huduma na mifumo, yenye lengo la kuhakikisha usalama, uhakika, tija na ufanisi katika takriban kila tasnia. Viwango ni njia ya mawasiliano baina ya mzalishaji na mtumiaji. Hutumika kama lugha inayounganisha pande mbalimbali, ikibainisha matakwa na vigezo vya ubora na usalama. Viwango huandaliwa na wataalamu wenye maarifa na ujuzi katika uwanja husika, ambao hukutana katika kamati mbalimbali za kitaalamu za uandaaji wa viwango.

### 1.5.2 Viwango hutayarishwaje?

Viwango hutayarishwa kwa kuleta pamoja pande zote zenye maslahi kama vile wazalishaji, watumiaji na wasanifu katika kila kifaa, bidhaa, mchakato au huduma. Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lina kurugenzi yenye dhamana ya kuandaa viwango. Katika kurugenzi hii kuna vitengo viwili na zaidi ya kamati za kitaalamu 100 za uandaaji wa viwango.

Viwango vingi huandaliwa kutokana na maombi ya sekta. Hata hivyo, maombi yanaweza kutoka kwa watu binafsi, kamati,

mashirika ya kitaalamu, umma au kutoka katika kitengo fulani ndani ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Maombi hupelekwa katika kurugenzi husika, kisha kurugenzi huwasilisha maombi hayo katika kamati husika au kuunda kamati mpya ya kitaalamu kulingana na maombi husika. Baada ya kamati ya kitaalamu kujiridhisha kuwa kuna haja ya kuandaa kiwango, mchakato wa uandaaaji kiwango huanza.

### 1.5.3 Faida za viwango

- a) Huweka usawa katika uwanja wa biashara;
- b) Huondoa mkanganyiko kuhusiana na bidhaa;
- c) Husaidia kufungua masoko zaidi;
- d) Hurahisisha biashara baina ya nchi na nchi;
- e) Hutoa uhakikisho wa ubora, usalama, kuaminika na ufanisi;
- f) Huipa serikali urahisi wa kuunda sheria zinazohusiana na masuala ya afya, usalama na uhifadhi wa mazingira;
- g) Hulinda afya na usalama wa walaji/watumiaji wa bidhaa mbalimbali.

### 1.5.4 Wapi na jinsi gani naweza kupata kiwango cha Tanzania?

Viwango vyote vya Tanzania hupatikana katika maktaba ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Aidha, machapisho yote ya viwango hupatikana katika tovuti ya TBS, [www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz) kupitia katalogi ya viwango iliyopo katikati juu katika ukurasa wa tovuti ya TBS. Unaweza kutafuta kwa jina, namba ya kiwango au namba ya ICS.



## 2.0 HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA SHIRIKA LA VIWANGO

Shirika la Viwango Tanzania linatoa huduma zifuatazo:

- a) Utayarishaji na uwianishaji wa viwango
- b) Upimaji
- c) Uhakiki wa vipimo
- d) Utekelezaji wa viwango
- e) Ukaguzi wa bidhaa
- f) Elimu kwa umma
- g) Udhibiti wa mifumo ya usimamizi ubora
- h) Udhibiti wa ubora wa bidhaa
- i) Mafunzo na Ushauri wa kitaalamu
- j) Usajili wa majengo ya chakula na vipodozi
- k) Usajili wa bidhaa za chakula na vipodozi
- l) Vinasaba
- m) Msaada wa kitaalam kwa wasafishaji na balozi inje ya nchi (TAE)

### 2.1 Huduma ya Udhibiti Ubora

TBS ina njia tatu za udhibiti wa ubora wa bidhaa.

#### 2.1.1 Matumizi ya Alama ya Ubora ya TBS

Skimu ya Alama ya Ubora ya TBS huwaruhusu wazalishaji wote ambao bidhaa zao zimepimwa na kuthibitishwa kukidhi matakwa ya viwango kutumia alama ya ubora ya TBS kwenye bidhaa zao. Alama ya ubora ya TBS hutumiwa na wazalishaji kwa ajili ya kutangaza bidhaa zao, huku walaji wakiitumia kama ushahidi kuwa bidhaa wanayotumiwa ina ubora unaotakiwa.

#### 2.1.2 Cheti cha Ubora

TBS pia ina utaratibu wa kuthibitisha ubora wa bidhaa kwa

kutumia viwango vya kampuni, vya kigeni au vya kimataifa vilivyothibitishwa na Kamati Maalumu, hususan pale ambapo hakuajwa na kiwango cha kitaifa cha bidhaa husika. Chini ya mpango huu, bidhaa hupimwa katika maabara za TBS kwa kuzingatia kiwango husika cha kampuni au cha kigeni au cha kimataifa na pia eneo la uzalishaji hukaguliwa na kuthibitishwa kuwa bora na salama.

### 2.1.3 Huduma ya uthibitishwaji mifumo ya usimamizi wa Ubora

Shirika La Viwango Tanzania hutoa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa mifumo ya usimamizi wa utoaji huduma katika taasisi, makampuni ya serekali na watu binafsi, kufuatana na matakwa ya kiwango cha kimataifa cha ISO/IEC 17021

Huduma hii inatolewa kwa taasisi na makampuni ya watu binafsi pamoja na serekali katika kuleta tija na ufanisi katika kutoa huduma bora ndani na nje ya nchi.

Huduma hii hutolewa na wakaguzi wa mifumo waliobobea na wenye uzoefu mkubwa na wamepata mafunzo ya kutosha katika nchi za Ujerumani, Uingereza, Dubai, Afrika ya Kusini pamoja na India.

Huduma ya uthibitishaji mifumo inayotolewa ni kama ifuatavyo;

- ISO 9001:2015 Mfumo wa usimamizi wa ubora
- ISO 14001:2015 Mfumo wa usimamizi wa mazingira
- HACCP- Mfumo wa usimamizi wa usalama wa chakula
- ISO 45001: 2018 Mfumo wa usimamizi wa usalama mahali pa kazi
- ISO 22000: 2018 Mfumo wa usimamizi wa usalama wa



chakula

- ISO 21001:2018 Mifumo ya Usimamizi wa Taasisi za Elimu (EOMS)
- ISO/IEC 17025:2017 Mahitaji ya Jumla ya Umahiri kwa Maabara za Upimaji na Ugezi
- ISO 15189 Mahitaji ya Ubora na Umahiri katika Maabara za Matibabu.
- ISO 50001:2018 Mfumo wa Usimamizi wa Nishati.

## 2.2 Upimaji na Metrolojia

Maabara za Shirika la Viwango Tanzania zilizazishwa mwaka 1982 ili kuwasaidia wazalishaji kuboresha bidhaa zao, kufanya upimaji wa bidhaa ili kuhakikisha kuwa zinafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa na kuthibitisha ubora wa bidhaa kabla ya kutoka na kuingia nchini.

TBS ina maabara Kumi na nne (14) zenye vifaa vya kisasa na wataalamu wa kutosha. Maabara hizo ni:

- a) Maabara ya Kemia;
- b) Maabara ya Uhandisi Ujenzi;
- c) Maabara ya Uhandisi Mitambo;
- d) Maabara ya Uhandisi Umeme;
- e) Maabara ya Kemia ya Chakula;
- f) Maabara ya Mikrobiolojia;
- g) Maabara ya Nguo na Ngozi;
- h) Kituo cha Teknolojia ya Ufungashaji.
- i) Maabara ya Metrolojia ya Jotoridi, Umeme, muda na Masafa
- j) Maabara ya Metrolojia ya Tungamo na ujazo
- k) Maabara ya Metrolojia ya Urefu
- l) Maabara ya Metrolojia ya Kemikali na Biolojia
- m) Maabara ya Metrolojia kimakanika
- n) Maabara ya ufanisi wa nishati

### 2.2.1 Maabara ya Kemia

Maabara hii ilianzishwa ili kutoa huduma za upimaji wa

bidhaa za kemikali na zile zenye muunganiko wa kemikali. Mfano wa bidhaa zinazopimwa katika maabara hii ni sabuni zote kwa aina zake, viuatilifu, maji, petroli na bidhaa nyingine mbalimbali.

### 2.2.2 Maabara ya Uhandisi Ujenzi

Maabara hii ina uwezo wa kupima bidhaa zinazotumika kwenye ujenzi kama vile matofali, mchanga, vigae, saruji, mbao, n.k. Pia maabara hii ina uwezo wa kupima ujenzi uliokamilika kama umefuata matakwa ya viwango au la.

### 2.2.3 Maabara ya Uhandisi Mitambo

Maabara hii hupima ubora wa mitambo na zana mbalimbali kama vile nondo, bati, pikipiki na vifaa na mashine mbalimbali ili kuangalia uimara, ustahimilivu na iwapo zana husika zinafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

### 2.2.4 Maabara ya Uhandisi Umeme

Maabara hii hupima ubora wa bidhaa za umeme kama vile nyaya, swichi, taa, soketi na vingine kadha wa kadha. Vifaa hivi huangaliwa kama viko kwenye ubora unaotakiwa ili visije vikaleta madhara kwa watumiaji.

### 2.2.5 Maabara ya Kemia ya Chakula

Maabara hii hupima ubora wa vyakula na bidhaa za kilimo. Maabara hii inapima kiasi cha kemikali, asidi, vitamini, unyevu, mafuta na maada nyingine kwenye bidhaa huweza kutambuliwa kupitia maabara hii.

### 2.2.6 Maabara ya Mikrobiolojia

Maabara hii hupima kiasi cha vijiumbe kinachopatikana katika bidhaa mbalimbali.



## 2.2.7 Maabara ya Pamba, Nguo na Ngozi

Hapa pamba, ngozi, nyavu, soli, nguo na bidhaa nyingine nyingi hupimwa. Kwa mfano kwa upande wa nguo, maabara hii huweza kubaini kama inachuja, inakunjikakunjika, uzito wake, kama ni pamba halisi na kadhalika.

## 2.2.8 Kituo cha Teknolojia ya Ufungashaji

Ufungashaji ni sehemu muhimu sana katika biashara. Katika ulimwengu wa viwango, bidhaa isiyofungashwa vizuri hukosa ubora. Ufungashaji si tu unatakiwa kutofautisha bidhaa moja na nyingine, bali pia unatakiwa uilinde bidhaa kwani bidhaa hupitia misukosuko mingi tangu pale inapozalishwa mpaka inapomfikia mlaji. Pia kila bidhaa ina kifungashio cha aina yake.

Kituo cha Teknolojia ya Ufungashaji (PTC) kina majukumu makuu manne kama ifuatavyo:

- a) Kusaidia na kuratibu maendeleo ya tasnia ya ufungashaji;
- b) Kutoa mafunzo kwa wazalishaji kuhusiana na teknolojia ya ufungashaji;
- c) Kudhibiti ubora wa nyenzo za kufungashia ikiwa ni pamoja na kutoa vyeti vya ubora kwa nyezo za kufungashia zilizotengenezwa kwa kuzingatia viwango vya Tanzania;
- d) Kutoa huduma ya upimaji wa nyenzo za kufungashia.

## 2.2.9 Maabara ya Metrolojia ya Jotoridi

Maabara hii inajihusisha na vifaa vinavyotumika kupima: Majokofu, Matanuru, Oveni, Incubators, Vifaa vya Kutakasia vyombo (*Autoclaves*), Majiko ya Umeme (*Hot Plates*), Vifaa vya kuchemshia vimiminika (*Liquid baths*), Hygromita, Chemba za unyevunyevu (*Humidity Chambers*) Humidifiers, Mita za Umeme, Vipima Ukinzani wa Umeme ardini (*Earth Resistance Testers*), Vipima Mkondo wa Umeme (*Ammeter*) Vipima nguvu Kuubwa na ndogo ya Umeme (*Voltmeter*), Chaja za Umeme, Vipima Muda (Saa) Vipima Kasi ya mzunguko (*Centrifuge, tachometer, Vortex, tachometer calibrator*), Masafa ya Radio.

## 2.2.10 Maabara ya Metrolojia ya umeme muda masufa

## 2.2.11 Maabara ya Metrolojia ya Tungamo na ujazo

Maabara hii hutoa huduma za unasabishaji na kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye maeneo ya Tungamo, Ujazo, Mgandamizo, Kani na Toki. Maabara hii pia inajihusisha na ugezi wa vifaa mbali mbali kama mizani ya aina zote, mawe ya kupima (*mass piece*) Flaski, Sirinji za sindano, Bureti, Silinda; Barometa, monita ya shinikizo la damu, Geji za mgandamizo aina zote, Mitambo ya Kushindilia zege, Toki renchi na vifaa ya kupima geji mbalilimbali.

## 2.2.12 Maabara ya Metrolojia ya Urefu

Maabara ya hii inajishughulisha na vifaa vinavyotumika katika kupima Urefu, Upana, Kina, Unene na Pembe. Maabara hii ina uwezo wa kupima vifaa vifuatavyo, futikamba, dip tape, rula, Geji ya skeli, *Feeler Gauge*, Seti ya *Gauge Blocks*, Penetromita, Geji ya Go-nogo, *Protractors*, *Filters*, Inklinomita ma Mraba wa mwashi



### 2.2.13. Maabara ya Metrologia ya Kemikali

Maabara hii ina uwezo wa kupima vifaa vifuatavyo Mita za kupima uwiano kati ya ujazo na uzito wa vimiminika (density meter and hydrometer) Mita za kupima kiwango cha pombe kwenye vimiminika (alcohol meter), Mita za kupima kiwango cha sukari kwenye vimiminika (refractomer), Mita za kusoma unyevunyevu kwenye mazao (moisture meter), mita ya PH na mita ya upitishi.

### 2.2.14. Maabara ya Metrologia ya Kemikali

Maabara ya Metrologia ya Mitambo hutoa ufuatiliaji wa vipimo (traceability), ulinganisho wa vipimo (inter-comparisons), na msaada wa kitaalamu katika vipimo vya nguvu, momenti (torque), na shinikizo. Pia inatoa huduma za uthibitishaji wa vipimo (calibration) kwa sekta mbalimbali, zikiwemo afya, utengenezaji, ujenzi, utalii, usafirishaji, anga, upimaji, taasisi za udhibiti, na taasisi za utafiti.

## 2.3 Mafunzo na Ushauri

Shirika la Viwango Tanzania lina Kitengo mahususi kwa ajili ya Mafunzo na Ushauri Uelekezi. Kitengo hiki huandaa na kutekeleza mafunzo viwandani na kutoa warsha kuhusiana na utekelezajiwa mifumo ya udhibiti ubora kwa kuzingatia viwango vya ISO 9001 (mfumo wa usimamizi wa ubora), ISO 14001 (mfumo wa usimamizi wa mazingira), ISO 22000 (mfumo wa uchanganuzi wa hatari na hatua muhimu za udhibiti) na ISO 17025 (mfumo wa usimamiziwa maabaraza upimaji na ugezi). Kozi nyingine huandaliwa kulingana na mahitaji ya mteja. Kozi hizo huwalengawafanyakaziwa viwandani wakiwamowatendaji wa kawaida, wasimamizi, mameneja na watendaji wakuu.

## 2.4 Usajili wa Majengo ya Chakula na Vipodozi

TBS husajili majengo/maeneo yanayohusika na biashara za vyakula na vipodozi kama machinjio, mabucha, maduka makubwa (supermarkets), maduka ya vyakula na vipodozi, wanaopika vyakula kwenye masherehe (caterers), mahoteli, migahawa, maghala na maeneo ya uzalishaji.

## 2.5 Usajili wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi

TBS husajili bidhaa za vyakula na vipodozi zinazozalishwa nje ya nchi na kuingizwa nchini. Bidhaa zinazokidhi viwango tu ndizo husajiliwa na kuruhusiwa kuingizwa nchini.

## 3.0 UTARATIBU WA KUPATA ALAMA YA UBORA

Zipo hatua mbalimbali ambazo mzalishaji hupaswa kuzizingatia kabla ya kupata leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS kwenye bidhaa yake.

### 3.1 Hatua ya Kwanza – Maombi

Maombi ya kupata alama ya ubora wa bidhaa hufanywa na muombaji kupitia mfumo wa kielektroniki (i-SQMT) unapatikana kupitia tovuti ya TBS ([www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)) kwenye kitufe cha e-service au moja kwa moja kupitia linki ya [https:// portal.tbs.go.tz](https://portal.tbs.go.tz)

Baada ya maombi kukamilika tarehe ya ukaguzi wa awali hupangwa. izingatiwe kuwa mwenye kiwanda anatakiwa kuwa katika uzalishaji siku ya kufanya ukaguzi wa awali.

### 3.2 Hatua ya Pili – Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wa awali hufanywa na wakaguzi wa TBS. Sampuli huchukuliwa na kupimwa ili kuona kama bidhaa inakidhi matakwa ya kiwango husika. Mkaguzi huandaa taarifa kuhusu hali halisi ya kiwanda na mambo yanayostahili kurekebisha.

### 3.3 Hatua ya Tatu – Upimaji

Sampuli zilizochukuliwa hupimwa katika maabara za TBS kwa kufuata kiwango husika. Baada ya kazi ya upimaji kumalizika, ripoti hutolewa kwa mwombaji.

### 3.4 Hatua ya Nne – Utoaji wa Leseni

Uamuzi kuhusu kutoa au kutotoa leseni ya kutumia alama ya ubora hutegemea tu ripoti ya ukaguzi wa awali wa kiwanda



pamoja na ripoti ya maabara. Kimsingi ripoti zote mbili zinatakiwa kuonyesha kwamba mazingira ya uzalishaji kiwandani, mfumo wa uzalishaji na bidhaa iliyopimwa havina matatizo.

Ikiwa sivyo basi mzalishaji hutakiwa kufanya marekebisho na baadaye mkaguzi wa TBS hutumwa tena na kuleta sampuli nyingine.

### 3.5 Muda wa leseni ya alama ya ubora

Leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS hudumu kwa mwaka mmoja na huhuishiwa baada ya kuhakikisha kwamba taratibu zilizokubalika zinafuatwa.

### 3.6 Gharama kwa wajasiriamali wadogo na wa kati

Serikali hutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia wajasiriamali wadogo na wa kati pale wanapoomba bidhaa zao wanazozialisha wenyewe zithibitishwe ubora.

### Ili kupata nafuu ya ada, mjasiriamali anatakiwa:

- Kupata barua ya utambulisho kutoka ofisi ya SIDO
- Kuwa na leseni ya biashara.

Wajasiriamali waliokwisha pata leseni ya kutumia alama ya ubora wanapaswa kutunza taarifa za uzalishaji na mauzo ambazo watatakiwa kuzionesha kwa wakaguzi wa TBS pindi zinapohitajika.

## 4.0 UTARATIBU WA USAJILI WA BIDHAA NA MAJENGO YA CHAKULA NA VIPODOZI

### 4.1. UTARATIBU WA USAJILI WA BIDHAA

TBS husajili bidhaa za vyakula na vipodozi zinazozalishwa nje ya nchi na kuingizwa nchini. Bidhaa zinazokidhi viwango tu ndizo husajiliwa na kuruhusiwa kuingizwa nchini.

#### 4.1.1 Hatua ya Kwanza – Maombi

Maombi ya usajili hufanyika katika mfumo wa kielektroniki unaopatikana katika tovuti ya TBS ([www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)) kwenye kitufe cha Huduma mtandao (e-service) halafu maombi ya huduma kwa njia ya mtandao (OAS). Mwombaji hutakiwa kujisajili katika mfumo na kisha kuingiza taarifa za bidhaa anazotaka kusajili.

#### 4.1.2 Hatua ya Pili – Malipo

Mwombaji hupewa gharama za kusajili bidhaa husika pamoja na namba ya kumbukumbu ya malipo ya serikali kupitia kwenye mfumo wa kielektroniki.

Baada ya malipo hutakiwa kuwasilisha sampuli katika ofisi za TBS.

#### 4.1.3 Hatua ya Tatu – Tathimini

Bidhaa hufanyiwa tathimini na mwombaji atapewa mrejesho kupitia mfumo wa kielektroniki (OAS) kama bidhaa imekidhi vigezo au la.

#### 4.1.4 Hatua ya Nne – Usajili

Bidhaa zinazokidhi vigezo husajiliwa na cheti cha usajili hutolewa kupitia mfumo wa kielektroniki.



## 4.2. UTARATIBU WA USAJILI WA MAJENGO

TBS husajili majengo/maeneo yanayohusika na biashara za vyakula na vipodozi kama machinjio, mabucha, maduka makubwa (supermarkets), maduka ya vyakula na vipodozi, wanaopika vyakula kwenye masherehe (caterers), mahoteli, migahawa, maghala na maeneo ya uzalishaji.

### 4.2.1 Hatua ya Kwanza – Maombi

Maombi ya usajili hufanyika katika mfumo wa kielektroniki unaopatikana katika tovuti ya TBS ([www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)) kwenye kitufe cha Huduma mtandao (e-service) halafu maombi ya huduma kwa njia ya mtandao (OAS).

Mwombaji hutakiwa kujisajili katika mfumo na kisha kuingiza taarifa za jengo analotaka kusajili na kuambatanisha picha za mchoro wa jengo, leseni ya biashara pamoja na ramani inayoelekeza jengo lilipo ili kuwezesha wakaguzi kulifikia.

### 4.2.2 Hatua ya Pili – Malipo

Mwombaji hupewa gharama za kulipia kulingana na aina ya shughuli anayofanya katika jengo husika pamoja na namba ya kumbukumbu ya malipo ya serikali kupitia mfumo wa kielektroniki.

### 4.2.3 Hatua ya Tatu – Tathimini

Baada ya malipo kufanyika Mkaguzi atafika kukagua jengo kulingana na vigezo vilivyowekwa ili kujiridhisha na kisha mwombaji atapewa mreji

### 4.2.4 Hatua ya Nne – Usajili

Jengo lililokidhi vigezo husajiliwa na cheti cha usajili hutolewa kupitia mfumo wa kielektroniki.



## 5.0 ORODHA YA BIDHAA ZILIZOPIGWA MARUFUKU KUTUMIKA

### 5.1. VIPODOZI VILIVYOZULIWA

#### 5.1.1 Maana ya Kipodozi

Kipodozi ni kitu kinachokusudiwa kutumiwa kwa amna ya kupaka, kumimina, kufukiza, kunyunyiza, kupuliza, au kutumiwa vinginevyo katika mwili wa binadamu au sehemu yeyote ya mwili kubadili muonekano.

#### 5.1.2 Aina za vipodozi

- I) Ngozi: Poda, rangi za midomo, rouge, krimu, losheni.
- II) Nywele: Sabuni za kuoshea nywele, dawa za nywele, kubadili rangi ya nywele
- III) Kucha; Rangi za kucha, kucha bandia na dawa ya kufuta rangi
- IV) Jicho: wanja, kope na mascara.

**NB:** Orodha ya Viambato vilivyopigwa marufuku tafadhali tembelea Tovuti: **[www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)**

### 5.2 BIDHA ZINGINE ZILIZOPIGWA MARUFUKU

|                             |                                                         |
|-----------------------------|---------------------------------------------------------|
| 1. Nguo za ndani za mitumba | 4. Matairi yaliyotumika                                 |
| 2. Mifuko ya plastiki       | 5. Tumbaku isiyovutwa                                   |
| 3. Mafuta ya breki DOT 3    | 6. Bidhaa za vipodozi zenye krimu za kung'arisha ngozi. |



## 6.0 UKAGUZI WA BIDHAA ZINAZOINGIA KUTOKA NJE YA NCHI (PVOC)

Shirika la viwango Tanzania (TBS) linatekeleza uhakiki wa utimizaji wa viwango vya bidhaa kwa ajili ya kudhibiti baadhi ya makundi ya bidhaa za matumizi kutoka nje ya nchi.

Uhakiki wa utimizaji viwango kabla ya usafirishaji wa bidhaa ni utaratibu wa uhakikiwa utimizaji wa viwango unaotumiwa kuhakiki kama bidhaa zitakazoingizwa kutoka nje ya nchi zinatimiza viwango stahiki vya taifa kabla ya kusafirisha bidhaa. Ni utaratibu wa uhakiki wa utimizaji viwango kwa bidhaa mahususi katika nchi zinazosafirisha bidhaa nje. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa kifungu 4(1) (s) cha Sheria Na 2 ya Viwango ya mwaka 2009

Kabla ya usafirishaji kuja Tanzania shehena zote zinazoshahiki PVOC ni lazima zipate hati za utoaji bidhaa forodhani na hati ya utimizaji viwango (COC) ambazo zikikosekana bidhaa zinazowasili kwenye Bandari za Tanzania zitakataliwa au kutozwa faini.

Uhakiki wa PVOC hufanywa na wakala nyingine zilizoidhinishwa, zinazofanya ukaguzi halisi ikijumuisha upimaji wa maabara, upitiaji wa nyaraka na ukaguzi wa viwanda pale ambapo ni muhimu.

### FAIDA ZA PVOC

- i) Hulinda afya, usalama na ulinzi watumiaji
- ii) Huzuia ushindani usio wa haki kutokana na bidhaa kutoka nje za viwango duni
- iii) Huwezesha utoaji bidhaa forodhani
- iv) Hutokomeza uteketezaji au gharama za kusafirisha tena nje bidhaa zenye viwango duni
- v) Huzuia Tanzania isiwe jalala la bidhaa duni

**NB:** Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea: [www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)



## 7. HITIMISHO

Shirika la Viwango Tanzania limepewa mamlaka ya kutoa bidhaa zenye ubora, hiyo ni pamoja na huduma ya viwango na uhakiki ubora kwa kufikia na kuvuka mahitaji ya wateja ili kuhifadhi uaminifu wa wateja katika bidhaa zitolewazo na Shirika. TBS inatumia rasilimali zake kuendelea kuboresha michakato yake ili kuhahikisha kwamba wafanyakazi wake wana uwezo wa kuhakikisha wanazalisha/wanatoa huduma zenye ubora na kwa wakati.

Hata hivyo Shirika linakumbana na changamoto mbalimbali kama vile uelewa mdogo wa wananchi kuhusu umuhimu wa bidhaa zilizothibitishwa, ambapo wengi wao hawajui umuhimu wa kutumia, kununua na kuuza bidhaa zilizothibitishwa na TBS, hivyo kusababisha ugumu kwa Shirika kufikia malengo yake ya kuondoa bidhaa hafifu sokoni. Ili kutatua changamoto hii, Shirika linatumia njia mbalimbali kama vile redio, televisheni, magazeti, mitandao ya kijamii na maonesho mbalimbali, pia Shirika limeanzisha kampeni ya kwenda kwa wadau wa bidhaa husika, mashuleni na maeneo ya wazi katika ngazi ya wilaya kutoa elimu, lengo likiwa ni kufikisha elimu kwa wananchi wote ili waweze kuelewa umuhimu wa viwango.

Shirika pia linafanya jitihada kubwa kuhakikisha linamfikia kila Mtanzania. Ili kufikia azma hiyo, Shirika limeongeza ofisi zake mipakani na kufungua ofisi katika kanda. Shirika lina namba ya simu ambayo ni huduma ya bure kwa wateja ambayo mteja anaweza kuitumia pale anapohitaji huduma kutoka TBS au pale anapohisi kuwa bidhaa aliyonunua haikidhi viwango. Namba hiyo ni **0800110827**



“Wajibu wa kuondoa bidhaa duni nchini ni wa kila Mtanzania”

**Kwa maelezo zaidi,wasiliana nasi kwa anwani  
zifuatazo:**

**MKURUGENZI MKUU**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

S.L.P. 9524, Dar es Salaam

Simu: +255 22 2450298 / 2450206 / 2451763-6

Hotline: +0800 110 827 / Nukushi: + 255 22 2450959

Barua pepe: info@tbs.go.tz / Tovuti: www.tbs.go.tz

Malalamiko: malalamiko@tbs.go.tz

**OFISI ZA KANDA:**

**NYANDA ZA JUU KUSINI**

(Iringa, Mbeya, Njombe and Songwe)

Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7, S.L.P. 1674 Mbeya, Tanzania

Simu: 025 2502848 / Nukushi: 025 2502848

**KANDA YA ZIWA**

(Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu and Shiyanga)

Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3, S.L.P. 1814 Mwanza, Tanzania

Simu: 028 2505044 / Nukushi: 028 2505044

**KANDA YA KASKAZINI**

(Arusha, Kilimanjaro, Manyara and Tanga)

Ngorongoro Tourist Center, Ghorofa ya 6, S.L.P. 2399 Arusha,

Tanzania Simu: 027 2520143 / Nukushi: 027 2520143

**KANDA YA KATI**

(Dodoma, Singida and Tabora)

Kambarage Tower, Ghorofa ya 6, S.L.P 2956, Dodoma, Tanzania

Simu: 026 2320310 / Nukushi: 026 2320310

**KANDA YA KUSINI**

(Lindi, Mtwara and Ruvuma)

Jengo la PSSSF, Sokoine House, Ghorofa ya 3, S.L.P 1396

Mtwara, Tanzania

Simu: 023 2334477 / Nukushi: 023 2334477

**KANDA YA MAGHARIBI**

(Katavi, Kigoma and Rukwa)

Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2, S.L.P 1276

Kigoma, Tanzania

Simu: 028 2804023 / Nukushi: 028 2804023

**KANDA YA MASHARIKI**

(Dar es Salaam, Morogoro na Pwani)

Jengo la PSSSF (Commercial Complex) Ghorofa ya 4, S.L.P

9425, Dar es Salaam





tbs

**“TUMIA BIDHAA ZILIZOTHIBITISHWA UBORA WAKE NA TBS”**





### **Cooperative Fuel Research Engine**

For determination of Research Octane Number (RON) in Fuel



**Premises Registration Permit**



***“The Home of Standards”***

***Mark applied on the product with a number for the  
relevant Tanzania Standard (TZS....)***

**Standards Mark of Quality**



***“Know the quality status of your  
products before buying them”***

## FOR MORE DETAILS CONTACT:

### Director General

Tanzania Bureau of Standards  
P. O. Box 9524, Dar es Salaam – Tanzania  
Tel: +255 22 2450206 / 2450949 / 245 0298  
Fax: +255-22-2450959 / Hotline: 0800110827  
E-mail: info@tbs.go.tz / Website: www.tbs.go.tz  
Complaints: complaints@tbs.go.tz

## TBS ZONAL OFFICES

**Southern Highlands Zone**  
(Rukwa, Mbeya, Njombe and Songwe)  
NHIF Building, 7th Floor  
Along Avenue Road  
P.O. Box 1674 Mbeya, Tanzania  
Tel: 025 2502848 / Fax: 025 2502848

**Eastern Lake Zone**  
(Mwanza, Mara and Simiyu)  
NSSF Building, 3rd Floor  
P.O. Box 1814 Mwanza, Tanzania  
Tel: 028 2505044 / Fax: 028 2505044

**Northern Zone**  
(Arusha, Kilimanjaro and Manyara)  
Ngorongoro Tourist Center, 6th Floor  
P.O. Box 2399 Arusha, Tanzania  
Tel: 027 2520143 / Fax: 027 2520143

**Western Lake Zone**  
(Kagera, Geita and Shinyanga)  
P.O. Box 816, Regional Commissioner Office,  
Magongo - Geita

**Southern Zone**  
(Mtware, Lindi and Ruvuma)  
PSSSF Building, Sokoina House, 3rd Floor  
P.O. Box 1396, Mtware, Tanzania  
Tel: 023 2334477 / Fax: 023 2334477

**Central Zone**  
(Iringa, Dodoma and Singida)  
Njedenywa Tower, 6th Floor  
P.O. Box 2956, Dodoma, Tanzania  
Tel: 026 2963865 / Fax: 026 2963865

**Western Zone**  
(Kigoma, Katavi and Tabora)  
NSSF Matao House Building, 2nd Floor  
P.O. Box 1276 Kigoma, Tanzania  
Tel: 028 2804023 / Fax: 028 2804023

**Eastern Zone Office**  
(Pwani, Morogoro and Tanga)  
Kibaha Town Council Office, Kibaha.

v. Prevents Tanzania from being a dumping ground for substandard goods.

**NB:** For more information please visit: [www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)

## 9. FUEL MARKING

Fuel marking is the introduction of a unique identifier (marker) in trace quantities into petroleum products at depots before distribution in the market. Markers are used to guarantee product integrity, as well as protect against counterfeiting, adulteration and tax fraud.

## 10. CONCLUSION

Tanzania Bureau of Standards (TBS) is mandated to deliver quality products that include standards and quality assurance services by meeting and even exceeding customers' requirements so as to retain their loyalty. TBS provides resources and continually improves her process to ensure that employees are capable of consistently producing quality products at the right time.

Although there are some few challenges like low public awareness on using certified products, which hinders the bureau's efforts to eradicate substandard products from the market, the Bureau is doing its best by providing education in different media outlets like radios, TV, newspapers, magazines and through various exhibitions and TBS campaigns to make sure that each and every individual is reached. As one of its initiatives, the Bureau has established new zonal offices to make sure that people are reached more easily. Also community radios are used in different regions for awareness programmes.

The Bureau is also has a HOTLINE through which the general public can call for free and report anything suspicious.

The hotline is 080 011 0827

**"The responsibility of free Tanzania from sub standards products it, s for us all"**

- i. Protects consumers' health, safety and security.
- ii. Blocks unfair competition from substandard imports.
- iii. Facilitates customs clearance.
- iv. Eliminates destruction or re-exporting costs for substandard goods.

### 8.1 Key Benefits

Before shipping to Tanzania all consignments subject to PVOC must obtain the mandatory custom clearance documents and certificate of conformity (CoC) without which the commodities arriving at Tanzanian Ports will be rejected or fined. The PVOC is carried out by authorized third-party agencies, consisting of physical inspection with combination of laboratory testing, documentary review and factory audits, where necessary.

for by section 4(1) (s) of the Standards Act No. 2 of 2009.

Pre-shipment Verification of Conformity (PVOC) is a conformity assessment procedure used to verify that products to be imported into Tanzania are in conformity with applicable national standards before shipment. It is conformity assessment and verification procedure to specific goods at exporting countries. It is provided for by section 4(1) (s) of the Standards Act No. 2 of 2009.

|                         |                                           |
|-------------------------|-------------------------------------------|
| 1. Used Undergarments   | 4. Used Pneumatic Tyres                   |
| 2. Plastic Carrier Bags | 5. Smokeless Tobacco Products             |
| 3. Lubricant DOT 3      | 6. Cosmetics Product with Whitenig creams |

### 7.2 Other Products Banned

**NB:** For list of prohibited Cosmetics substances please visit [www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)

xvi. ISO 37001:2025 Anti-Bribery Management System

xvii. ISO 29001:2020 Petroleum, Petrochemical and Natural Gas Management System

xviii. ISO 18788:2015 Management System for Private Security Operations.

The aforementioned programmes are conducted on behalf of TBS by qualified personnel with skills and experience in relevant programmes. The programmes are designed and implemented to promote an understanding of the requirements of the key certification and accreditation standards. Implementation of these programmes neither is a pre-condition nor does guarantee certification by TBS. In addition, TBS does not give specific advice for the development of business operations for the sake of maintaining impartiality principles.

## **7.0 BANNED PRODUCTS**

### **7.1 BANNED COSMETICS**

#### **7.1.1 Meaning of Cosmetics**

A cosmetic is an item intended to be rubbed, poured, sprinkled or sprayed on, introduced in to or otherwise applied to the human body or any part thereof for cleansing, beautifying, promoting attractiveness or altering the appearance

#### **7.1.2 Categories of cosmetics**

- i. Skin: Powder, lipstick, rouge, cream, lotion, and solution
- ii. Hairs: Shampoo, conditioner, creams, bleach, coloring preparation
- iii. Nails: Nail lacquers, lacquers removers

iv. Teeth: Powder, paste, gel and dentifrices

v. Eye: Eyeliner, mascara, eye shadow and Eyebrow pencil

## 6.4 Technical Assistance

TBS offers technical assistance on certification issues in terms of awareness programmes, understanding of standard requirements and internal auditing programmes in the following international Standards;

- i. ISO 9001:2015 Quality Management Systems (QMS)
- ii. ISO 22000:2018 Food Safety Management Systems (FSMS)
- iii. HACCP - Hazard Analysis and Critical Control Points.
- iv. ISO 21001:2018 Educational Organization Management Systems (EOMS)
- v. ISO 14001:2015 Environment Management Systems (EMS)
- vi. ISO 45001:2018 Occupational Health and Safety Management systems (OH&SMS)
- vii. ISO 50001:2018 Energy Management System
- viii. ISO 21001:2018 Educational Organization Management Systems (EOMS)
- ix. ISO 14001:2015 Environment Management Systems (EMS)
- x. ISO 45001:2018 Occupational Health and Safety Management systems (OH&SMS)
- xi. ISO/IEC 17025:2017 General requirements for the competence of testing and calibration laboratories
- xii. ISO 15189 Requirements for quality and competence in medical laboratories.
- xiii. ISO 50001:2018 Energy Management System
- xiv. ISO 22301:2019 Business continuity Management System
- xv. ISO 27001:2022 Information Security Management System

### 6.3 Management system certification application procedure

- a. Ability to maintain consistency
  - b. Increase in customer's confidence
  - c. Enhance customer's satisfaction
  - d. Identify and address the risks and opportunities associated with organization.
  - e. Ability to demonstrate conformity to Compliance with necessary statutory and regulatory requirements
  - g. Increase in competitive advantage
  - h. Improved top management's commitment and decision-making.
  - i. Improved working conditions and motivation for employees.
